Kulisha Akili,
Kupambana na Njaa
www.feedingminds.org
fmfh@ fao.org

????TC/D/Y2735P/1/3.03/10000

Kulisha Akili, Kupambana Na Njaa

ULIMWENGU USIO NA NJAA

Dunia Isiyo na Njaa

Mtizamo wetu ni kuwepo kwa dunia isiyokuwa na njaa na ukosefu wa lishe bora – Dunia ambayo kila mtu ana hakikisho la chakula wakitakacho ili kuwa na afya bora. Mwono wetu ni dunia inayotoa na kulinda heshima ya kila binadamu wake wote. Hii ni dunia ambamo watoto wote wanaweza kukua, kusoma, na kusitawi, na kuendelea hadi kuwa watu wenye afya na watu wenye kujali maslahi ya wengine katika jamii.

Kumekuwepo na mafanikio katika kupunguza njaa na ukosefu wa lishe bora duniani, hata hivyo hatujafanikiwa kuwa na ulimwengu ambao watu wote hawasumbuliwi na njaa. Tunaona kuwa elimu na habari kwenye masuala yanayohusu njaa ya ulimwengu, kuwepo kwa chakula, na lishe bora kuwa mambo yatakayofanikisha ukweli huu. Kwa hivyo tunakita nguvu zetu kwa vijana na waalimu wao. Ikiwa kila mwaka watoto kote duniani watatangulizwa kwa pamoja kwa makala tofauti yanayofundisha kuhusu njaa na ukosefu wa lishe na kinachohitajika kufanywa wakati wa siku ya chakula duniani (16 Oktoba) wanaweza kukua wakielewa utegemeano wa dunia ikiwa watafundishwa masomo kutoka sehemu mbalimbali za dunia, hasa kutoka tamaduni mbalimbali na hali, watakuwa tayari kushirikiana katika kutatua matatizo ya njaa na ukosefu wa vyakula? Kuna njia yoyote ambayo kwayo kikundi cha vijana kinaweza kufundishwa ili kujenga uraia wa kidunia wenye dhima.

Tunaamini kuwa majibu kwa maswali haya yote ni “NDIYO”. Kama walimu mko katika nafasi nzuri na bora kuwaeleza vijana jinsi ya kujali na kuingia mapambano dhidi ya njaa. Makisio, mawazo na nguvu za vijana vinawakilisha hazina muhimu ya kuendeleza jamii na mataifa yao. Nyinyi waalimu wao mnaweza kusaidia katika kuleta mabadiliko kupitia utoaji wa habari, kushirikiana katika habari, kuhimiza kushiriki na kuonyesha vijana kuwa wana jukumu muhimu la kutekeleza katika kupata dunia isiyo na njaa.

Tunawahimiza nyinyi kuungana na waalimu na wanafunzi kote duniani kushiriki katika *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa*.

Utangulizi wa Mwalimu *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa*

NANI: Waalimu kote duniani watakaopenda kuwatanguliza wanafunzi wao kwa matatizo ya njaa na ukosefu wa lishe wanaweza kutumia makala ya Kulisha Akili, *Kupambana na Njaa* na miongozo yake kwa masomo.

NINI: *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa* imepangwa kuwa hatua ya mwanzo ya waalimu kuanzisha somo la njaa katika ulimwengu kwa wanafunzi wao. Kwa sababu ya matatizo mbalimbali, tamaduni na mazingira tofauti katika ulimwengu mzima, masomo yamepangwa kama kiunzi cha waalimu huku kukiwa na mazingatio kuwa waalimu watahitaji kurekebisha mipaka yake, lugha, mazungumzo na shughuli zilizotolewa ili kukidhi haja na matarajio ya mazingira ya wanafunzi wao. Viwango vyote vinahusu mada ya ni nini njaa na lishe bora, na ni nani wenye njaa? Ni kwa nini watu wana njaa na kukosa lishe bora na tufanye nini ili tusaidie kumaliza njaa? Kila somo lina malengo yake, dhana, na shughuli zitakazowashughulisha wanafunzi iko katika mijadala kuhusu matatizo haya makubwa na yenye kutokea kila mara.

Masomo matatu yanatolewa kwa viwango vikuu vya elimu vya shule: Cha msingi, kati na upili. Masomo yameelekezwa kati ya maendeleo ya ujuzi ya kila kiwango kinachohusika. Kwa sababu gredi tofauti na umri mbalimbali wa wanafunzi zinafasiriwa kwa njia tofauti kote ulimwenguni, waalimu watahitaji kufanya uchaguzi wa makala zinazofaa viwango vya wanafunzi wao na maendeleo ya bongo zao, huku wakifanya marekebisho yapasayo.

LINI: Siku ya chakula duniani, Oktoba 16 na mwaka mzima wanafunzi kote ulimwenguni wanaweza kutumia masomo haya ili kuielewa njaa na ukosefu wa lishe vizuri zaidi. Waalimu wanaweza basi kutoa mawazo yanayotokana na madarasa yao maalum ili waalimu wengine wapate kutumia kote ulimwenguni katika siku zifuatazo za chakula ulimwenguni. Mawazo mapya, shughuli na masomo kutoka kote ulimwenguni yatakusanywa na kusambazwa kila mwaka.

WAPI: Katika darasa lako na katika madarasa mengine maelfu duniani kwa wakati mmoja.

KWA NINI: Mtizamo wetu ni dunia ambapo kila mtu ana chakula cha kutosha ili kuishi maisha yenye afya na yenye kufana bila kuwa na ukosefu wa lishe. Tunaamini elimu na habari kwa masuala yanayohusu njaa ya ulimwengu, kuwepo kwa chakula, na lishe bora kama mambo ya kimsingi kuufanya mwono wa dunia kuwa kweli. Lengo ni kuzua darasa la dunia ambapo watoto na vijana kote watasema na kujadili masuala mamoja, kwa matarajio ya kuwaandaa na kuwasisimua kushiriki katika shughuli ili kujenga ulimwengu usio na njaa.

VIPI: Unahimizwa kunakili na kutumia makala haya wakati mzima katika mwaka shuleni, huku ukichukua masomo na kuyaelekeza katika mahitaji na hali maalum ya wanafunzi wako na vifaa vya darasani. Masomo yanayochukuliwa na kuendelezwa katika eneo husika fulani yanayohusu jamii mahsusi ndiyo yenye kufaa zaidi.

Masomo ya vielelezo yamepangwa kufundishwa dakika 45 kwa kila mojawapo, hata hivyo yanaweza kufundishwa kwa kina kabisa au kijuujuu, upendavyo, kukidhi haja za darasa lako. Habari za kimsingi zinatolewa kwa kila somo na dhana za kutumia ama na wewe mwenyewe na wanafunzi wako, kutegemea utakavyo. Kila somo lina shughuli zinazopendekezwa na hoja za mjadala ambazo unaweza kuzitumia zilivyowasilishwa au unaweza kuzirekebisha ukizitumia kama msingi na mwongozo ili kuzua shughuli zako kwa kila mada.

Vifaa vyote vya Kulisha Akili, Kupambana na Njaa *vinapatikana pia katika mtandao. Barua memo: www.feedingminds.org*

Ili kushiriki maoni yenu na masomo tafadhali tazama eneo la maoni mwishoni mwa kitabu. Mtando wetu: fmfh@fao.org

Kama walimu kote duniani ni vizuri kuamua kifaacho katika tamaduni mbalimbali na mazingira tofauti na kuanza kuyatumia masomo haya ipasavyo, kuanzishwa mfululizo wa vifaa vifaavyo vya kufundishia masuala ya njaa. Tungependa kupokea maoni yenu kuhusu masomo haya na hasa tungependa wewe ushiriki na wengine katika marekebisho uliyofanya. Hali hii itatusaidia sisi kurekebisha programu hii mwaka hata mwaka. Vile vile unahimizwa kuwasilisha masomo au matokeo kutoka madarasa yako yanayoweza kutumiwa na wengine kote ulimwenguni kuhusu mradi huu wakati wa siku ya chakula duniani mwaka ujao (huwa tarehe 16 Oktoba).

Kuhusu Siku ya Chakula Duniani

Siku ya chakula Duniani husherekewa kila tarehe 16 Oktoba ili kuadimisha kuanzisha kwa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), 1945. Nia ya Siku hiyo ni kutoa changamoto kwa umma juu ya maisha ya wenye njaa na ukosefu wa lishe bora, kwa kuwahiza watu ulimwenguni kote kuchukua hatua dhidi ya njaa. Mataifa zaidi ya 150 duniani huadimisha siku hii kila mwaka. Katika Umoja wa Mataifa zaidi ya mataifa 450, yakiwa ya kibinafsi, mashirika ya kujitolea yaliyodhaminiwa na Siku ya Chakula Duniani pamoja makundi ya kienyeji huwa changamoto kwa karibu ya kila jamii. Kwa mara ya kwanza siku hii ilifanyika mwaka 1981, na tangu hapo Siku ya Chakula Duniani imekuwa na mada pekee inayolenga maudhui maalum. Mada ya mwaka 2000, ilikuwa ni “Milenia ya Dunia isiyo na Njaa” Maudhui ambayo yametokana na miaka ya awali ni “Vijana dhidi ya Njaa” (1999) na “Wanawake Kulisha Dunia” (1998).

Changamoto inayohusiana ni kampeni ya Chakula-Habari, ambayo inahusisha matangazo ya televisheni, radio, sarakasi na matendo mbalimbali ili kutoa ujumbe mahsusi ya kuwa wakati umefika wa kufanya vitendo kuhusu janga la njaa duniani. Lengo la Chakula-Habari ni kutoa msisimko wa kushirikisha rasilimali ndogo ndogo kwa ajili ya miradi midogo itakayowapa uhakika wa chakula. Michango inayotolewa kwa ajili ya Chakula-Habari, husaidia mamia ya miradi midogo midogo katika nchi zinazoendelea ili kuwasaidia wakulima wadogo kupanda chakula kingi au kwa kuongeza mapato kwa ajili ya kununulia chakula cha kutosha kuwalisha familia yao. Makala ya maudhui ya Siku ya Chakula Duniani/Chakula-Habari ya karibuni yanapatikana katika mtandao wa FAO.

Njaa na Ukosefu wa Lishe Bora Duniani

Ili kuwa na afya na mchangamvu, inatupasa kuwa na chakula cha kutosha, bora na sampuli tofauti ili kutosheleza mahitaji ya nguvu na yale ya madini. Watoto hawawezi kujijenga kikamilifu bila lishe bora na hata watu wazima watapata matatizo katika kudumisha uwezo wao.

Siyo kila mmoja anaweza kupata chakula anachokihitaji na hali hii imesababisha njaa kwa kiasi kikubwa pamoja na ukosefu wa lishe bora duniani. Takribani watu milioni 800 wana utapiamlo mbaya na hawawezi kupata chakula cha kutosha cha kuwapa nguvu za kimsingi. Takribani watoto milioni 200 walio na umri wa chini ya miaka mitano huwa na madhara na ishara za ukosefu wa lishe bora wanapokuwa na ukosefu wa chakula kwa kipindi fulani na wakati wa njaa, na wakati wa mizozo ya kijamii idadi hii huongezeka. Kwa mujibu wa makadirio fulani ukosefu wa lishe bora ni sababu kuu inayosababisha vifo vya takriban watoto milioni 13 walio chini ya umri wa miaka mitano wanaokufa kwa sababu ya magonjwa ya kawaida yanayoweza kuzuilika kama ukambi, kuhara, malaria numonia, au mchanganyiko wa haya magonjwa.

Sehemu kubwa ya watu wenye utapiamlo huishi katika Asia na Pasifiki. Hili ni eneo ambalo lina asilimia sabini ya jumla ya watu katika mataifa yanayoendelea na ina theluthi mbili (Milioni 526) ya watu wenye utapia mlo. Katika nchi ya India pekee kuna watu milioni 204 wenye utapiamlo na eneo la kusini la Asia lina zaidi ya thuluthi moja (milioni 284) ya jumla ya watu wa aina hiyo duniani. Aasilimia nyingine 30 ya watu (milioni 240) huishi Kusini Mashariki mwa Asia na Asia Mashariki ambapo zaidi ya watu milioni 164 ya watu bilioni 1.2 wa China wana utapiamlo. Takriban robo moja ya watu wenye utapiamlo huishi katika Afrika chini ya jangwa la sahara ambalo ndilo eneo lenye kiwango kikubwa cha watu wenye utapiamlo. Hali hii ni mbaya sana katika sehemu ya Afrika ya Kati Mashariki na Kusini mwa Afrika ambapo kuna asilimia 44 wa jumla ya watu wana utapiamlo.

Ukosefu wa lishe bora ndiyo sababu kubwa ya kimsingi ya uzani wa chini wa watoto wakati wa kuzaliwa na ukuaji mbaya. Watoto wenye uzani wa chini wanapozaliwa huwa na matatizo ya ukuaji na magonjwa katika kipindi chao cha utoto, ujana, hadi katika uzima na wanawake waliokuwa na matatizo ya ukuaji huenda wakaendeleza hali hii ya ukosefu wa lishe bora kwa kuzaa watoto wenye uzani wa chini. Uhusiano baina ya ukosefu wa lishe wakati wa ujana – pamoja na kipindi cha kukua mtoto tumboni – na maendeleo ya baadaye maishani, afya mbaya na magonjwa kama ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa sukari, na presha ya damu unaanza kuzuka. Watoto milioni 30 wanazaliwa kila mwaka na matatizo ya kiafya yanayosababishwa na ukosefu wa lishe bora tumboni.

Ukosefu wa lishe bora unaotokana na vitamini muhimu madini muhimu unaendelea kusababisha maradhi mabaya au hata vifo miongoni mwa mamilioni ya watu kote ulimwenguni. Zaidi ya watu bilioni 3.5 wameathiriwa na ukosefu wa madini ya ayani na bilioni 2 wamo katika hatari ya ukosefu wa madini ya ayodini na milioni 200 ya watoto wasiokwenda shuleni wameathiriwa na ukosefu wa vitamini A. Ukosefu wa Ayani unaweza kusababisha matatizo ya ukuaji, upambanaji dhaifu dhidi ya magonjwa na matatizo ya muda mrefu ya maendeleo ya shaksiya na matatizo katika utendakazi wa uzazi, inachangia takriban asilimia 20 ya vifo vinavyohusiana na uleaji wa mimba. Ukosefu wa ayodini unaweza kusababisha uharibifu wa ubongo kabisa, matatizo ya ukuaji, matatizo ya uzaaji, kupunguza kupona kwa watoto tezi. Mama mja mzito anapokuwa katika hali ya ukosefu wa ayodini hali hii inaweza kusababisha hali mbalimbali za matatizo ya ukuaji kwa mtoto wake. Vitamini A inapokosekana hali hii husababisha upofu au vifo miongoni mwa watoto, inachangia vile vile ucheleweshwaji katika ukuaji wa mwili na kusababisha kuzorota kwa uwezo wa mwili kupigana na magonjwa, na matokeo yake ni kuongezeka kwa vifo miongoni mwa watoto wachanga.

Hata kiasi kidogo cha dosari hizi huweza kuzuia maendeleo ya mtoto na uwezo wa kusoma wakati wa ujana wake, na kusababisha kufanya vibaya shuleni, na matokeo yake ni watoto wengi kuondoka shuleni na kuwa na mzigo wa watu wasiosoma. Matokeo mabaya zaidi ya kiafya ya hali hizi tatu ya ukosefu wa lishe bora yanaweza kupunguza kuwepo kwa chakula cha kutosha na vyakula vya aina mbalimbali yanayotoa vitamini muhimu pamoja na madini.

Katika nchi nyingi, matatizo ya kiafya yanayohusiana na wingi wa vyakula bora ni tisho linaloongezeka. Kunona kupita kiasi wakati wa uchanga na ujana ni hali inayohusishwa na matatizo mbalimbali ya kiafya na kuendelea kwake hadi cukubwani husababisha madhara ya kiafya tangu kuongezeka kwa uwezekano wa vifo vya mapema hadi hali za kudhoofisha na ambao huathiri kizazi. Matatizo haya yanayozuka siyo ya nchi zilizoendelea tu bali kuna nchi zinazoendelea zinazokabiliwa na matatizo haya mawili ya utapiamlo na upungufu wa vyakula na magonjwa yanayohusiana na vyakula vilivyozidi. Pia vyuma vizito na dawa za kunyunyizia wadudu ni kizuizi kikubwa cha uboreshaji wa lishe bora katika kila nchi duniani. Matatizo yanayoletwa kupitia vyakula ni mengi katika mataifa mbalimbali, na watoto ndio wahasiriwa wa mara kwa mara- watoto wanapoharisha na kusababisha upungufu wa uzani na kiwango kikubwa cha vifo vya watoto wachanga.

Hata kama ni kwa kiwango kidogo au katika hali zake mbaya sana matokeo ya utapiamlo na afya husababisha hali mbaya katika viwango vya maisha na maendeleo mabaya ya uwezo na kibinadamu. Ukosefu wa lishe bora huweza kusababisha hasara katika kuzalisha mali na hasara za kiuchumi kwa kuwa watu wazima walioathiriwa na hali ya ukosefu ya lishe bora na athari nyingine hawawezi kufanya kazi kikamilifu; hasara za kielimu, kwa kuwa watoto hudhoofishwa au kuugua kiasi cha kutoweza kwenda shuleni au kusoma vizuri, gharama za kiafaya maana inabidi kunguza watu wanaougua maradhi yanayosababishwa na magonjwa yanayotokana na ukosefu wa lishe bora; na vile vile gharama za kuangalia na kutunza walemavu na wakati mwingine familia zao.

Katika karne iliyopita, kulikuwa na juhudi kubwa katika kuongeza siyo idadi ya chakula tu bali ubora wake na kuongeza hali ya kiafya ya watu. Huku utoaji wa vyakula duniani ukienda sambamba na ongezeko la idadi ya watu, na afya, elimu na huduma za kijamii zimeboreka kote duniani kwani idadi ya wenye njaa na wanaokosa lishe bora imepungua kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo kupata vyakula mbalimbali vya kutosha na visivyo na madhara bado ni tatizo kubwa katika nchi mbalimbali, hata pale pasipo na chakula cha kutosha katika kiwango cha taifa. Katika kila nchi aina moja au nyingine ya ukosefu wa lishe na njaa huendelea kuwepo kwa mfumo tofauti.

Kumaliza njaa huanza tu pale ambapo kuna chakula cha kutosha kinachozalishwa na cha kutosha kwa kila mtu. Hata hivyo, kupanda chakula cha kutosha hakumaanishi njaa yaweza kumalizwa. Uwezekano wa watu wote nyakati zote kupata chakula bora cha kutosha na kisicho na madhara kwa maisha yenye afya – usalama wa chakula lazima uwepo.
Ongezeko la juhudi almradi kuhakikisha kuwepo kwa chakula zinahitajika ili kumaliza njaa na hali ya ukosefu wa lishe bora na athari zake mbaya miongoni mwa vizazi vya sasa na vijavyo; kote duniani. Mchango wa kila mmoja wetu kupitia kubadilishana kwa habari, kujali na kushiriki katika shughuli – ni muhimu katika kuhakikisha ni haki ya kila binadamu kuwa huru kutokana na njaa.

Tarama pia karatasi ya Siku ya Chakula Duniani na masuala Mbalimbali "Kikwi kisicho na Njaa" Hupatikana katika hali iliyochapwa na pia kwenye Mtandao www.fao.org

Washiriki katika *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa*

Mradi wa *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa* ulianzishwa na kundi la vyama vya kimataifa visivyo vya kiserikali ambavyo vimeungana pamoja ili kusaidia kumaliza njaa na ukosefu wa lishe bora kupitia elimu. Washiriki wanaamini katika kuja pamoja katika ushirikiano wa nguvu na ujuzi na dunia isiyo na njaa inaweza kupatikana kwa haraka na kwa mafanikio badala ya kila shirika kufanya kazi pekee yake.

Shirikisho la Waalimu wa Kimarekani

Shirikisho la Kimarekani la Waalimu ni Chama Cha wafanyikazi kinachowakilisha zaidi ya wanachama Milioni moja katika nyanja za elimu K-12 (Waalimu na walio kama wataalam) Serikali za nchi, elimu ya juu na vyama vya wauguzi na taaluma za utabibu. Shirikisho la AFR lilianzishwa mnano mwaka wa 1916 na linajulikana kwa maadili ya kidemokrasi na kazi nzuri kwa niaba ya wanachama wake, na athari kubwa kwa viwango na mienendo ya kitaalamu katika mahali pa kazi wanachama.

555 New Jersey Avenue NW, Washington, DC 20001-2079, USA
Simu: (+1) 202 879 4490 - Kipepesi (faksi): (+1) 202 393 8648
Ukurasa wa mtandao: www.aft.org

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO)

FAO ilianzishwa mnamo mwaka wa 1945 na lengo la kuinua viwango vya lishe bora na maisha, kuongeza uzalishaji wa kilimo na kuboresha hali ya maisha ya wakazi wa mashambani. FAO ina wafanyikazi kote duniani na ina wananchi wanachama 180. Jumuiya ya Ulaya na FAO hulenga kupunguza ufukara na njaa kwa kuendeleza maendeleo ya kilimo, lishe bora na kutafuta kuwepo chakula cha kutosha – chakula kipatikane kwa watu wote wanapokihitaji kwa maisha bora.

Viale delle Terme Di Caracalla, 000100 Rome Italy
Mtu wa kuwasiliana naye: Valeria Menza, Kitengo cha Chakula na lishe bora
Simu: (+39) 06 5705 4292 - Kipepesi: (+39) 06 5705 4593
Ukurasa wa mtandao: www.fao.org

Mavuno ya wakati ujao

Mavuno ya wakati ujao hulenga kujenga dunia yenye kiasi cha chini cha umaskini, familia ya binadamu yenye afya bora watoto wenye afya nzuri na mazingira bora kwa kuongeza kiwango cha uelewa na kuunga mkono juhudi za utafiti wa kisayansi. Husaidia kuleta matokeo ya utafiti kwa jamii za mashambani katika nchi zinazoendelea na pia kufanya juhudi kusomesha watoto na watu wazima kuhusu umuhimu wa kilisha dunia na kulinda ulimwengu.

PMB 238 2020 Pennsylvania Ave NW Washington,
DC, 20006-1846, USA
Simu: (+1) 202 473 3553
Ukurasa wa mtandao: www.futureharvest.org

Chuo cha Kimataifa cha Sera ya Chakula (IFPRI)

Azimio la IFPRI ni kutambua na kutathmini mikakati ya kitaifa na kimataifa na sera za

kutosheleza mahitaji ya chakula ya nchi zinazoendelea kwa kiwango kinachoweza kudumishwa, huku wakizingatia zaidi nchi zenye chumi ndogo, watu maskini na usimamizi bora wa mali za asili ambazo ndizo mhimili wa kilimo.

2033 K Street NW, Washington, DC 20006-1002 U.S.A
Simu: (+ 1) 202 862 5600
Ukurasa wa mtandao: www.ifpri.org
Orodha: www.ifpri.cgiar.org/new/newatfpri.htm

Elimu ya Kimataifa na Ungamo (iEARN).

iEARN ni ungamo la kimataifa la elimu la mawasiliano linalohusisha shule na vikundi vya vijana katika zaidi ya nchi 90 ili kuwezesha wanafunzi kuelewa teknolojia za Mtandao kwa miradi ya pamoja ya masomo kwa kushughulikia masuala ya kitaifa na kimataifa.
iEARN-usa
475 Riverside Drive #540, New York, NY 10115, USA
Simu: (+1) 212 870 2693 - Kipepesi: (+1) 212 870 2672
Ukurasa wa mtandao: www.iearn.org

Shirika la Kujitolea la Kitaifa (NPCA)

NPCA ni shirika lisilo la kifaida la watu wa kujitolea, wafanyikazi wa awali na rafiki wa Shirika la Kijitolea miradi na programu za NPCA zinalenga “kuiregesha dunia nyumbani” kupitia shughuli za elimu ya dunia, kujenga amani, huduma na utetezi wa kimataifa.

1900 L Street NW, Suite 205, WashingtoN, DC 20036, U.S.A
Simu: (+1) 202 293 7728 - Kipepesi: (+1) 202 293 7554
Ukurasa wa mtandao: www.rpcv.org

Mradi wa Elimu wa Newsweek (NEP)

Azimio la Nep ni kuendeleza kushiriki kwa wanafunzi katika masuala ya siku hizi. Mradi huu unalenga kuboresha ujuzi wa wanafunzi wa uchambuzi wa sera ya umma na kuongeza kushiriki kwao katika mambo na shughuli za kitaifa. NEP hutoa seti za magazeti ya Newsweek kwa shule za upili na madarasa ya vyuo katika lugha ya Kiingereza, Kijamii, Uchumi na ESL. Bei nafuu za wanafunzi pekee huzingatiwa kwa dazani ya makala kama vile ramani, maswali miongozo ya waalimu, vijitabu vya rejea na makala ya kujenga ujuzi.

SLP 919 Mountain Lakes, NJ 07046,USA
Simu/Kipepesi - Ndani ya Marekani: 800 526 2595
Simu/Kipepesi - Nje ya Marekani: (+1) 212 445 5032
Ukurasa wa mtandao: www.school.newsweek.com.

Chama Cha Umoja wa Mataifa Cha Elimu, Sayansi, na Utamaduni (UNESCO)

UNESCO huendeleza umoja na ushirikiano kati ya mataifa kupitia elimu ya sayansi, utamaduni na mawasiliano ili kuheshimu zaidi haki, utawala unaozingatia sheria na haki za binadamu na uhuru halisi unaosisitizwa na Mwafaka wa Umoja wa Mataifa. UNESCO hufanya kazi na waalimu katika viwango vyote na Vyama vingine ili kujumlisha elimu ya kisayansi na kitamaduni na kusaidia wanafunzi kuelewa mazingira yao, chaguzi zao za kijamii na kibinafsi ili kuwezesha kuwepo maendeleo.

7 Place De Fontenoy, Paris 07 SP, France 75352
Mshirikishaji: Anna-Maria Hoffman-Barthes
Kipepesi: (+3) 1 4568 5622
Ukurasa wa mtandao: www.Unesco.org

Kamati ya Kitaifa ya Kimarekani ya Siku ya Chakula Duniani.
Siku ya Chakula Duniani ni shughuli ya kila mwaka duniani ambayo nia yake ni kuongeza uelewa, mwaka mzima, wa muda mrefu wa masuala tata ya kuhakikisha kuwepo kwa chakula kwa kila mtu. Kamati ya Kitaifa ya Kimarekani ni muungano wa vyama vya kibinafsi 450 vya kitaifa visivyo vya kifaida vilivyo nchini Marekani.

2175 K Street NW, Washington, DC 20437 U.S.A
Mshirikishaji: Patricia Young, Mshirikishi wa Kitaifa
Simu: (+1) 202 653 2404 - Kipepesi: (+1) 202 653 5760
Ukurasa wa mtando: www.worldfooddayusa.org

Benki ya Dunia
Benki ya Dunia ndilo shirika kubwa duniani lenye kusaidia katika maendeleo na hutoa wastani wa dola bilioni 20 zikiwa kama mikopo ya kila mwaka kwa nchi zinazokopeshwa. Benki hii inatumia raslimali zake za kiuchumi, wafanyaikazi wake wenye ujuzi wa hali ya juu na elimu yake kubwa kusaidia kila nchi katika usitawi unaoweza kudumishwa kuhakikisha kuwa kuna ugawaji sawa. Dhima yao kubwa ni kusaidia watu na nchi maskini zaidi. Katika mandeleo ya mashambani kuna mambo yafuatayo!

1. Kuongeza uzalishaji wa kilimo, kutoa kazi na kuwepo kwa chakula cha kutosha mashambani.
2. Kujenga miundomsingi kama barabara, mabwawa ya maji, shule na hospitali, na kutoa huduma za kijamii kwa watu wa mashambani; na
3. Kusaidia kuendeleza maendeleo ya mashambani yanayoambatana na mazingira na eneo fulani.

1818 H Stree NW. Washington DC 20433, USA
Mtu wa kuwasiliana naye: Lynn R. Brown, MC 5110
Simu: (+1) 202 458 8175 - Kipepesi: (+1) 202 522 3307
Ukurasa wa mtandao: www.worldbank.org

Washiriki **Arab Nutrition Society, Asia-Pacific Network For Food and Nutrition, Secretariat of the Pacific Community, Federación Latinoamericana de Asociaciones Académicos de Nutrición y Dietética, Fundación de Vida Rural - Universidad Católica de Chile, Colegio de Profesores de Chile, Kenya Coalition for Action in Nutrition, Southern Africa Teachers' Organisation, Società Italiana di Nutrizione Umana, European Food Information Council, Associated Schools Project Network, World Association of Girl Guides and Girl Scouts.**

Kudhamini *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa*

Kila kazi kuhusu *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa* imefanywa na washiriki wa miradi. Ili kufika katika madarasa yote kote duniani, usaidizi zaidi unahitajika kwa sababu ya tafsiri, usanifu, vifaa vya darasani, kuchapa na kusambaza. Zaidi ya hayo utoaji wa vifaa kwa matumizi ya baadaye katika Siku za Chakula Duniani kutahitaji msaada zaidi. Ikiwa ungependa kudhamini au kuchangia kwa njia moja fulani katika kutayarisha vifaa hivi na kuvifanya vipatikane kwa kiasi kikubwa, tafadhali wasiliana na mmoja katika washiriki katika *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa*.

Shukrani

Washiriki katika *Kulisha Akili, Katika Kupambana na Njaa* wanapenda kushukuru kwa michango iliyotolewa na watu binafsi ambao walitoa usaidizi wao kwa mradi huu. Kwa maendeleo ya mradi na yaliyomo, Valeria Menza, FAO. Kwa kuusimamia mradi, twapongeza Patricia Young, Kamati ya kimarekani ya Kitaifa ya Siku ya Chakula Duniani. Kwa utayarishaji na uandaaji wa miongozo ya masomo pongezi ni kwa Claudia Probart, mtaalamu aliyetembelea FAO.

Shukrani zinatolewa kwa Christine Terry, Stephanie Kempf, Jane Levine na Lary Levine kwa ajili ya michango yao kwa miongozo ya masomo.
Pia shukrani za dhati ni kwa kituo cha Habari za Kilimo (WAICENT)/FAO kwa kufanya ukurasa wa mtandao, kwa Chiara Caproni kwa michoro ya shule za msingi, kwa Davies Zulu, msanii wa Zambia kwa michoro, na kwa Todd Metroken wa Supon Design, Inc, kwa mambo ya *Kulisha Akili, Kupambana na Njaa* na michoro ya jalada.

Kazi ya wanachama wa kamati ndogo inapongezwa. Hawa ni: Anne Baker, National Peace Corps Association, Everlyne Banda, IFPRI; Lynn Brown, Benki ya Dunia ; William D. Clay, FAO; Valeria Menza, FAO; Connie Cordiovilla, AFT; AnnaMaria Hoffman-Barthes, UNESCO, Susan Linyear, National Peace Corps Assocation; Frank Method, UNESCO, Dave Milburn, Newweek Education Program; Deborah Parker, ambaye awali alikuwa Newsweek Education Program; Mandy Tumulty, Peace Corps, na Claus vonGrebmer, IFPRI.

H